BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

OROGHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 17 Mei, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

a) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
b) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
c) Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
d) Ukaguzi wa Taarifa ya Kitaalamu ya CAG Kuhusu Utekelezaji wa Ujenzi na Utengenezaji wa Majengo ya Skuli Unguja na Pemba.
e) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi Cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
f) Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) na Miradi ya Maendeleo ya Wadi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.
g) Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara**

**Maalum za SMZ:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Kamati ya PAC Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

a) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
b) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
c) Ukaguzi wa Taarifa ya Kitaalamu ya CAG Kuhusu Utekelezaji wa Ujenzi na Utengenezaji wa Majengo ya Skuli Unguja na Pemba.
d) Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) na Miradi ya Maendeleo ya Wadi Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Hotuba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

a) Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
b) Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
c) Kwa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

98. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kunahitajika matunzo mahsusi katika Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Zanzibar, zikiwemo Ofisi ya Rais, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (OMKR) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, mazingira, uingiaji na utokaji wa wenyeji na wageni katika OMKR si wa kuridhisha na ni hatarishi.

(a) Je, ni lini Serikali itaipa OMKR hadhi na mazingira yanayokidhi haja.

(b) Je, ni kwa nini uingiaji na utokaji wa wenyeji na wageni katika OMKR haulingani wala haufanani na wa Ofisi nyengine za viongozi wakuu na ni wa kutia mashaka.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kujenga jengo la OMKR linaloendana na hadhi ya Ofisi hiyo.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

30. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika suala la kujiongezea kipato na kupunguza umasikini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeamua kujenga masoko pamoja na majengo mbali mbali katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Je, ni utaratibu gani utakaotumika katika kuwapatia wananchi milango au sehemu za kufanyia biashara katika majengo hayo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

67. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni benki ya wananchi kama inavyojulikana nchi nzima, lakini huduma zinazotolewa na benki hii zinawakimbiza wateja wake.

(a) Je, kuna sababu gani za kiufundi zinazowapelekea wateja kuikimbia benki yetu ya PBZ.

(b) Je, Wizara yako inafuatilia vipi kwa karibu malalamiko ya wananchi wengi dhidi ya wahudumu wa benki yetu hii, ili waweze kutoa huduma bora kama wanavyosifiwa wahudumu wa benki nyengine.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

118. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kama inavyokumbukwa kwamba Serikali iliwaongezea mishahara wafanyakazi wa umma tokea mwezi Julai, 2022 na kutoa maelekezo kwa sekta binafsi nayo kufanya hivyo. Hata hivyo, inasikitisha kwamba sekta binafsi imechelewa sana kutekeleza agizo hilo.

(a) Je, ni kwa nini sekta binafsi haikutekeleza maelekezo ya Serikali kwa wakati, kama ilivyofanya Serikali kwa watumishi wake.

(b) Je, ni lini sekta binafsi itaanza kuwalipa watumishi wake mishahara mipya kama ilivyoelekezwa na Serikali.

(c) Je, ni kwa nini Serikali inazitaka taasisi binafsi kulipa kiwango maalum cha ujira kwa vibarua ilhali Serikali yenyewe inalipa chini ya kiwango hicho.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

76. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika changamoto zinazokikabili Chuo Cha Kiislamu Pemba, ni ufinyu wa makaazi ya wanafunzi ikiwa ni pamoja na mabweni ya kulala wanafunzi hao.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inaifahamu changamoto hii.

(b) Je, Wizara yako itachukua hatua gani kuiondoa changamoto hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

53. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wa Shehia za Chimba na Kinowe wanategemea sana huduma ya maji safi na salama kutoka kisima cha Pombwe. Hata hivyo, bado wana changamoto kubwa ya kuipata huduma hiyo kwa uhakika kutokana na ukosefu wa tenki pamoja na kuchelewa kusafishwa kwa kisima hicho.

(a) Je, Serikali ina mpango wa kuwajengea tenki wananchi hawa ili waweze kupata huduma hii kwa uhakika.

(b) Je, ni utaratibu upi unaotumika wa kuvisafisha visima kwa wakati.

**Wizara ya Afya:**

100. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na changamoto katika utaratibu wa kusafirisha wagonjwa wanaopewa rufaa kutoka Pemba kuja kuendelea na matibabu Unguja, ikiwa ni pamoja na wagonjwa wasio na uwezo kulazimishwa kujisafirisha kwa gharama zao pamoja na kuwasafirisha madaktari au wauguzi wanaoambatana nao kwa gharama za wagonjwa au jamaa zao, wakati mwengine zikiwemo gharama za kuwalipa posho ya kujikimu wafanyakazi wa Serikali wanaolazimika kuambatana na wagonjwa hao.

(a) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na huduma hii.

(b) Kwa vile katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kumeibuka madalali kwa jina la "*madaktari wastaafu*" ambao huwarubuni wagonjwa kulipia fedha nyingi ili kuwapatia tiba ambayo Serikali inaitoa bure na kwa wakati sahihi, je, ni ipi juhudi ya Serikali kulidhibiti hili na hatua gani imewahi kuzichukua.

(c) Je, kwa mwaka 2021 - 2022, ni wagonjwa wangapi pamoja na watumishi wa Serikali waliowasindikiza waliosafirishwa kwa gharama za Serikali kutoka Pemba kuja Unguja na kutoka Unguja kwenda Tanzania Bara.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

8. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwepo na msongomano mkubwa bandarini Malindi hasa pale meli zinapotoka Pemba au zinapofunga gati, boti au meli mbili kwa wakati mmoja. Hali hii inapelekea usumbufu mkubwa kwa abiria na kukosekana umakini katika ukaguzi wa abiria na mizigo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua jambo hili kwa haraka ili kuepusha kutokezea madhara na kuwawezesha wananchi kusafiri bila ya kupata usumbufu wowote.

(b) Je, Wizara inasemaje kuhusiana na kuwepo kwa maegesho ya kutosha bandarini hapo, ili kukwepa usumbufu uliopo.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

132. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Moja kati ya mambo yanayotia wasiwasi ni kuukuza utalii bila ya kuwashirikisha wazawa katika kila hatua na daraja, jambo ambalo linaleta athari hasi katika jamii. Hali hiyo imeanza kujitokeza kwa kasi katika maeneo yenye mahoteli na zaidi yanayomilikiwa na kuendeshwa na wawekezaji wasio wazawa.

(a) Je, Serikali inadhibiti vipi athari hasi za utalii kwa lengo la kuulinda utamaduni wa Mzanzibari.

(b) Je, Serikali ina mipango na mikakati ipi iliyo rasmi na madhubuti ya kuimarisha utalii wa kimaumbile na

mazingira (eco-tourism), ili kuendana na maazimio ya kimataifa ya utalii endelevu uliojengwa katika nguzo za uhifadhi wa mazingira.

(c) Je, ni hatua zipi za kinidhamu na kisheria kwa miaka mitano ya karibuni zilizochukuliwa na kutekelezwa dhidi ya waliokiuka masharti ya uendeshaji wa huduma ya utalii Zanzibar yakiwemo masharti la kutunza maadili ya Mzanzibari na uhifadhi wa mazingira.

## III. KAULI YA SERIKALI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa:

a) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
b) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
c) Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
d) Ukaguzi wa Taarifa ya Kitaalamu ya CAG Kuhusu Utekelezaji wa Ujenzi na Utengenezaji wa Majengo ya Skuli Unguja na Pemba.
e) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi Cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.
f) Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) na Miradi ya Maendeleo ya Wadi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.
g) Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2022.

IV. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
17 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA